**MKATABA WA KUUZIANA SHAMBA LILILOPIMWA LENYE NA. YA UKA:124IR/MKG/130 NA HATI MILKI NA.124IRA-94388, KATIKA KIJIJI CHA ISUPILO, KATA YA LUMULI, KITONGOJI CHA MAKANYAGIO-WILAYA YA IRINGA.**

**Mkataba** huu umefanyika leo tarehe ...23... / ...08.../2025

**KATI YA**

**ADAM CAESAR POPPE NA KLAUS CAESAR POPPE** wa S.L.P 408, **IRINGA, TANZANIA** (ambao ni Ndugu katika mkataba hu una wote kwa pamoja watajulikana kama "**WAUZAJI**") kwa upande mmoja.

**NA**

**FU XUAN TRADING COMPANY LIMITED** (ambayo ni kampuni iliyosajiliwa kisheria na yenye **TIN NA: 186-305-868** yenye eneo la biashara Makumbusho-Dar Es Salaam ambapo katika mkataba huu itajulikana kama "**MNUNUZI**") kwa upande mwingine.

**KWAKUWA, WAUZAJI** ni wamiliki halali wa shamba hilo kwa asilimia 50% kwa 50% wa hisa, lenye nambari ya usajili **124IRA/MKG/130** na lenye namba ya **Hati ya Hatimiliki: 124IRA-94388** lililopo **Isupilo,** Katika Kata ya **Lumuli**, Kitongoji cha **Makanyagio**- Wilaya ya Iringa lenye ukubwa wa **Ekari Kumi na Tano na pointi Tatu Nane Saba (15.387),** Na kwamba Muuzaji ambapo wote wanamiliki asilimia 50% kwa 50% kwa hiari yao wenyewe na bila kushurutishwa na upande wowote wameamua kuuza shamba hilo kwenye kampuni ifahamikayo kama **FU XUAN TRADING COMPANY LIMITED,** ambayo ndio **MNUNUZI.**

**NA KWAKUWA Mnunuzi** bila kushurutishwa na upande wowote amekubali kununua shamba hilo lenye namba ya usajili kwa matumizi ya uwekezaji wa kiwanda.

**HIVYO BASI INAKUBALIWA HAPA NA PANDE ZOTE MBILI KATIKA MKATABA HUU KAMA IFUATAVYO: -**

A-C.P /K-C.P

1. **Kwamba** Muuzaji kwa hiari yake amekubali kuuza shamba hilo lenye ukubwa wa **Ekari Kumi na Tano na pointi Tatu Nane Saba (15.387),** kwa gharama ya **Shilingi Milioni Ishirini na Tatu Elfu Themanini na Mia Tano tu (Tshs: 23,080,500/=)** ikiwa ndio gharama ya uuzaji.

2. **Kwamba** Mnunuzi amekubali kununua shamba hilo kwa bei tajwa hapo juu kwa masharti yaliyomo katika mkataba huu.

3. **Kwamba,** Wauzaji na Mnunuzi wamekubaliana kwamba Mnunuzi atakabidhiwa shamba husika mara tu baada ya pande zote mbili kusaini makubaliano haya kwa makubaliano zaidi kwamba, Mnunuzi awe amelipa pesa yote kama gharama ya shamba hilo lenye nambari za usajili.

4. **Kwamba,** imekubaliwa zaidi katika Mkataba huu kuwa Mnunuzi mara tu baada ya kusaini makubaliano haya, watakuwa na haki ya kuendeleza shamba husika ikiwa ni pamoja na kulitumia shamba hilo kwa matumizi ya uwekezaji wa kiwanda.

5. **Kwamba,** Wauzaji awnathibitisha shamba hilo ni la kwao binafsi, na halina mgogoro wa aina yoyote wala halijawekwa rehani mahali popote iwe kwa taasisi ya fedha wala mtu binafsi kwa sababu yoyote ile.

6. **Kwamba,** endapo Mnunuzi atabaini shamba hilo limewekwa rehani au kuuzwa kwa mtu mwingine, basi Wauzaji ndiyo watatakiwa kuwajibika kulipa rehani hiyo na gharama nyingine zozote zitakazojitokeza na kukabidhi shamba hilo kwa Mnunuzi likiwa halina mgogoro wa aina yoyote.

7. **Kwamba,** baada ya mauziano ya shamba hilo, Mnunuzi ndio atakuwa mmiliki halali wa shamba hilo, Na kwamba atakuwa na haki ya kisheria ya kuuza ila kwa kufuata utaratibu wa sheria za ardhi na **TIC**, kuweka rehani shamba hilo kwa mtu yeyote au taasisi yoyote ya fedha. Na Wauzaji wanaahidi kutoa ushirikiano katika kubadilisha umiliki wa majina ya shamba hilo tajwa hapo juu.

A-c-P|K-c-P

8. **Kwamba,** mkataba huu utalindwa, kutetewa na kusimamiwa na Sheria za Mikataba pamoja na sheria nyingine za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MKATABA HUU UMETIWA SAINI NA WAHUSIKA WA PANDE ZOTE MBILI PAMOJA NA MASHAHIDI WAO NA KUSHUHUDIWA LEO TAREHE ...23... MWEZI ...08... MWAKA ...2025...**

**UMESAINIWA hapa MAFINGA-IRINGA** na
**ADAM CAESAR POPPE**
Ambaye anatambulika kwangu rasmi leo
**Tarehe...23...Mwezi...08... Mwaka, 2025.**

..........[signature]..........
**MUUZAJI**

**UMESAINIWA hapa MAFINGA-IRINGA** na
**KLAUS CAESAR POPPE**
Ambaye anatambulika kwangu rasmi leo
**Tarehe...23...Mwezi...08... Mwaka, 2025.**

.....K.C. POPPE.....
**MUUZAJI**

**SHAHIDI WA MUUZAJI**

1. JINA: **NINAH ADOLF KIRSCHSTEIN**
   SAHIHI: ......N.Adolf......

**MBELE YANGU:**

**JINA:** ......MAURICE S. MWAMWENDA......
**SAHIHI:** ......M.S MWAMWENDA......
**ANUANI:** ......S.L.P 13495, DSM......
**WADHIFA:** ......WAKILI......
**TAREHE:** ......23-08-2025......

**UMESAINIWA hapa MAFINGA-IRINGA** na
**FU XUAN TRADING COMPANY LTD**
Ambaye anatambulika kwangu rasmi leo
**Tarehe...23...Mwezi...08... Mwaka, 2025.**

..........................
**MNUNUZI**

FU XUAN SHUN TRADING COMPANY LIMITED ★ DAR ES SALAAM ★ P.O. Box 42450

A.C.P / K.C.P

**KWA NIABA YA KAMPUNI:**

**JINA:** Wang kun

**SAHIHI:** 王坤

**ANUANI:** Makumbusho - Dar-es-salaam.

**WADHIFA:** Msimamizi mkuu

**SHAHIDI WA MNUNUZI**

1. JINA: **DU HUI**

   SAHIHI: 杜辉

**MBELE YANGU:**

**JINA:** MAURICE S. MWAMWENDA

**SAHIHI:** M.S MWAMWENDA

**ANUANI:** S.L.P 13495, DSM

**WADHIFA:** WAKILI

**TAREHE:** 23 - 08 - 2025

Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

A.C.P / K.C.P